**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI NI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO TAREHE 24/10/2021**

**Wajumbe waliohudhuria**

1. Ndg. Shehemba Kuziwa - Mwenyekiti wa bodi
2. Ndg. Bonifasi Soko - Katibu
3. Dr. John Mwingira - Mjumbe
4. Dr. John Assey -Mjumbe
5. Adv. Ellah Msingwa - Mwalikwa
6. Ndg. Andrew Marco - Mwalikwa

**Wajumbe wasiohudhuria**

Elinaza Kiswaga -kwa taarifa

**Sekretarieti**

1. Ndg. Rustica Dugange - Mwandishi wa Mikutano

## KDC/ZAB/01/2022 KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuhudhuria kikao, Aidha aliwataka kushiriki kikamilifu katika kujadili agenda zilizopo mbele yao. Alifungua kikao saa 07:30 Mchana

## KDC/ZAB/02/2022 KURIDHIA AGENDA

1. Kufungua kikao
2. Kuridhia agenda
3. Kuridhia kutumia single source miradi ya uvico.19,kwa mafundi [ local fundi] na ununuzi wa saruji.
4. Kutangaza zabuni za ujenzi na umaliziaji wa miradi kama ifuatayo

- Ujenzi wa jengo la wodi ya wazazi lenye chumba cha upasuaji kituo cha afya Ruaha Mbuyuni.
- Ujenzi wa jengo la maabara kituo cha afya Ruaha mbuyuni

- Ujenzi wa wodi ya watoto katika hospitari ya wilaya ya kilolo
- Ujenzi wa jengo la Maabara katika kituo cha Afya ng`uruhe
- Umaliziaji wa zahanati ya mlafu
- Umaliziaji wa zahanati ya Ikuka
- Ukarabati wa zahanati ya Itimbo
- Umaliziaji wa jengo la upasuaji katika hospitari ya wilaya ya kilolo
- Umaliziaji wa madarasa mawili ya shule ya msingi Ihimbo

**KDC/ZAB/01/2022/ KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 4:30 asubuhi kwakuwakalibisha wajumbe katika kikao hicho pia aliwataka wajumbe wawewasikivu na wawe huru katika kuchangia hoja mbalimbali

**KDC/ZAB 02/2022 KURIDHIA KUTUMIA FORCE ACCOUNT KATIKA MIRADI YA UVICO.19**

Ilielezwa kuwa halmashauri ya wilaya ya kilolo imepokea fedha za miradi ya Uvico.19 Tsh.1,460,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa vyumba (73) sabini na tatu vya madarasa katika shule za sekondari, 240,000,000/= ujenzi wa vyumba vya madarasa (12) katika shule za msingi (*shule shikizi*). Tsh. 90,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya watumishi (Three in one) na Tsh. 250,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ICU Katika hosipitali ya Wilaya ya kilolo. Kwamba miradi hii itikelezwe kwa njia ya Force Account. Aidha baada ya majadiliano ya kina wajumbe wote walikubaliana kuwa utekelezaji huo uendelee kwa njia ya Force Account kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni mbalimbali za manunuzi.

Hosptali ya Wilaya, Ujenzi wa wodi ya watoto katika Hospitali ya Wilaya ya Kilolo, Ujenzi wa jengo la maabara kituo cha afya Ng'uruhe, Ujenzi wa nyumba ya watumishi (Tatu kwa moja) kituo cha afya Ruaha Mbuyuni.

Baada ya kuwasilishwa wajumbe walishauri miradi yote itangazwe ndani ya siku saba za kisheria na tangazo libandikwe kwenye mbao za matangazo kuanzia tarehe 07/02/2022.

Adha Mganga Mkuu wa Wilaya aliomba kuongeza miradi ifuatayo; umaliziaji wa zahanati ya Mlafu, umaliziaji wa zahati ya Ikuka, ukarabati wa zahanati ya Itimbo. Alijibiwa kuwa hawezi kuwasilisha kwasababu taarifa hajafika kitengo cha manunuzi na BOQ haijaandaliwa

**KDC/ZAB/03/2022 MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

Hiki ni kikao halali kinatakiwa kiwe na muhtasari uliosainiwa na Mwenyekiti na katibu, ambapo ilielezwa kuwa kila kikao cha wazabuni huwa ni zima moto hivyo basi ajitahidi kuwa mpangilio mzuri kwenye kikao cha zabuni

Aidha Fundi aliyekuwa anajenga jengo la kuhifadhia maiti anasumbua hivyo watangaze upya, ilielezwa kuwa hamwezi kutangaza upya wakati alisimama kutokana na changamoto za kukosa fedha kutoka Halmashauri. Wajumbe walitaka fundi huyo aitwe ili ahojiwe kuwa anaridhia kuendelea na kazi au la

**KDC/ZAB/.04/2022 KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa mahudhurio yao na kuwaomba yale yote yaliyoagiza yafanyiwe kazi. Alifunga kikao saa 8:30 mchana

**UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| **JINA** LUWANGA MLOMO | **JINA** JOSEPH NSWILLA |
| **SAINI** [signature] | **SAINI** [signature] |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

15.11.2021

**TAREHE**

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO
## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO TAREHE 28/10/2021

**Wajumbe waliohudhuria**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Anna M. Msola | - D/K/Ilula | -Mwenyekiti |
| 2. | Ndg. Elinaza Kiswaga | - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji | -Katibu |
| 3. | Mhe. Hezron J. Nganyagwa | - D/K/ Ihimbo | - Mjumbe |
| 4. | Mhe. John S. Mkonda | - D/K Irole | -Mjumbe |
| 5. | Mhe. Amini J. Tengelakwi | - D/K/Dabaga | -Mjumbe |
| 6. | Mhe. Fabiola S. Nzasule | - D/V/M/T/Mazombe | -Mjumbe |
| 7. | Mhe. Rashid R. Nzelemela | - D/K/Ruahambuyuni | -Mjumbe |

**Wajumbe Wasiohudhuria**

1 Mhe. Justin L. Nyamoga – Mbunge-kwa taarifa

**Wataalamu waliohudhuria**

| | |
|---|---|
| 1 Ndg. Amelye L. Mfugale | - Afisa Utumishi (W) |
| 2. Ndg. Ako Tluway | - Mweka Hazina (W) |
| 3. Ndg. Shehemba Kuziwa | - Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W) |
| 4. Ndg. Hassan Ussi | - Mkaguzi wa ndani (W) |
| 5. Ndg. Alto Kinunda | - Mthibiti Ubora wa Shule (W) |
| 6. Ndg. Issa Kibuga | - Kny Afisa TEHAMA na Uhusiano (W) |
| 7. Dr. John Assey | -. Mganga Mkuu (W) |
| 8. Ndg. Venance Mwaikambo | - Mratibu wa TASAF |
| 9. Ndg. Boniface Soko | - Afisa Manunuzi (W) |
| 10. Ndg. Bernard Kajembe | - Kny. Afisa Ardhi, Maliasili na Mazingira (W) |
| 11. Ndg. Loyce Mgonja | - Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 12. Ndg. Alloys Maira | - Afisa Elimu Msingi (W) |
| 13. Ndg. Scholastica Gibore | - Afisa Maendeleo ya Jamii (W) |
| 14. Ndg. Edward Mbembe | - Afisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ilula |
| 15. Adv. Ellah Msigwa | - Mwanasheria (W) |
| 16. Ndg. Lucas H Daud | - Afisa Mipango (W) |
| 17. Eng. Emmanuel Sigachuma | - Kaimu Mhandisi Ujenzi (W) |
| 18. Ndg. Filemon Namwinga | - Afisa Uchaguzi (W) |
| 19. Ndg. Laiton Ngamilo | - Katibu TSC (W) |
| 20. Dr. John Mwingira | - Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |

**Sekretarieti**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Freedom Wimmo | Mwandishi wa Kikao |
| 2. | Ndg. Rustica Dugange | Mwandishi wa kikao |

**KDC/FUM/AG.92/2021 KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuhudhuria kikao, Aidha aliwataka kushiriki kikamilifu katika kujadili agenda zilizopo mbele yao. Alifungua kikao saa 6:36 Mchana

**KDC/FUM/AG.93/2021 KURIDHIA DONDOO ZA AGENDA**

Dondoo za Agenda ziliwasilishwa na kupokelewa na wajumbe kama zinavyoonekana hapa chini:-

1. Kufungua kikao.
2. Kuridhia agenda
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe 16/09/2021
4. Yatokanayo na Muhtasari wa kikao cha kawaida cha kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe16/09/2021
5. Kujadili Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwezi Septemba, 2021.
6. Kujadili taarifa ya Mkaguzi wa Ndani kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2021
7. Kupitia na kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli za idara kwa kipindi cha robo ya kwanza kwa mwezi Julai hadi Septemba 2021
   I Miradi ya Maendeleo
   II Kitengo cha Manunuzi
   III Kitengo cha Sheria
   IV Kitengo cha TEHAMA
   V Idara ya utumishi na utawala
8. Taarifa ya Mapokezi ya Fedha ya UVIKO-19 za miradi ya Maendeleo
9. Mapendekezo ya kumlipa posho ya Madaraka Afisa Mtendaji wa Mamlaka Mji Mdogo Ilula
10. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti
11. Kufunga kikao.

**KDC/FUM/AG.94/2021 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 16/09/2021**

Muhtasari uliwasilishwa na kupokelewa na wajumbe, ambapo walikubaliana kuwa yaliyosomwa ndiyo yaliyojadiliwa katika kikao na hivyo Muhtasari ulisainiwa pamoja na masahihisho na kuwekwa kuwa kumbukumbu sahihi ya Halmashauri.

**KDC/FUM/AG.95/2021 YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 16/09/2021**

Taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya kikao kilichopita iliwasilishwa na kupokelewa. Wajumbe waliridhia taarifa ya yatokanayo iliyowasilishwa. Aidha wajumbe walihitaji kumjua mzabuni aliyepatikana kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya Tarafa ya Mazombe kwa jina ambapo, Afisa Manunuzi alijibu kuwa mzabuni ni Ndugu Jonson Adick, wa S.L.P 1215, Iringa.

- Kitengo cha manunuzi kifuatilie fedha alizolipwa M/S Charles chavala (Mzabuni) za vifaa kwa ajili ya ujenzi wa choo cha mnada wa masukanzi na machinjio ya ilula na mrejesho uletwe katika kikao kijacho.
- Mafunzo kwa mabaraza ya kata yafanyike kabla ya robo ya pili 2021/2022 kuisha
- Kamati imeagiza kufanyika kwa mafunzo ya mabaraza ya kata kabla ya robo ya pili 2021/2022 kisha
- Yafanyike matengenezo kwenye vyoo vya jengo la Halmashauri ya Wilaya ya kilolo

**KDC/FUM/AG.99/2021 TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA UVICO. 19 TSH. 2,040,000,000/= ZA MIRADI YA MAENDELEO**

Ilielezwa kuwa halmashauri ya wilaya ya kilolo imepokea kiasi cha fedha Tsh. 2,040,000,000/= fedha za miradi ya Uvico.19 kwa mchanganuo ufuatao Tsh.1,460,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa vyumba (73) sabini na tatu vya madarasa katika shule za sekondari, 240,000,000/= ujenzi wa vyumba vya madarasa (12) katika shule za msingi (*shule shikizi*). Tsh. 90,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya watumishi (Three in one) na Tsh. 250,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ICU Katika hosipitali ya Wilaya ya kilolo. Kwamba miradi hii itikelezwe kwa njia ya Force Account. Aidha baada ya taarifa kupokelewa wajumbe walihoji juu wa wana nchi kuchangia ujenzi wa madarasa ambapo wameshauri itumike njia ya uhamasishaji kwa wananchi kushiriki katika kuchangia mawe,matofari (Benki ya matofari), na mchanga ili taratibu za ujenzi zianze mapema kwa kufuata sheria,taratibu na kanuni mbalimbali za manunuzi.

KDC/FUM/AG.101/2021 MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI

Hapakuwa na mengineyo.

KDC/FUM/AG.102/2021 KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti aliwashukulu wajumbe kwa michango ya mawazo walio toa. Aidha alishukulu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Uongozi wa Mhe. Samia Suluh Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha za miradi katika Halmashauri ya wilaya ya kilolo ambayo itawagusa wananchi wengi. Pia aliipongeza menejimenti kwa kazi nzuri zinazo endelea katika Halmashauri nakusisitiza yale yaliyoagizwa na kamati yafanyiwe kazi. Alifunga kikao saa 09:58 Alasiri

**UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| **JINA** HEZRON NGANYAGWA | **JINA** DR. JOHN MWINGIRA |
| **SAINI** Nganyagwa | **SAINI** Mwingira |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

25.11.2021

**TAREHE**